

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA USIMAMIZI YA HALMASHAURI YA
MJI HANDENI (CMT) KILICHOFAANYIKA TAREHE 19/10/2021 KATIKA UKUMBI
WA HALMASHAURI YA MJI HANDENI KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA ZA
KAMATI YA FEDHA KWA ROBO YA KWANZA 2021/2022**

WATAALAMU WALIOHUDHURIA

- | | | |
|----------------------------|---|--|
| 1. Bi. Maryam A. Ukwaju | - | Mkurugenzi wa Mji |
| 2. Bw. Boniface Maday | - | Kny.Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 3. Bi. Aldegunda Matunda | - | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji |
| 4. Bw. Toba Mhina | - | Mkuu wa Idara ya Mazingira |
| 5. Bw. Fred C. Mpondachuma | - | Kny.Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 6. Bw. Wilbard Sakaya | - | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. Bw. Zakaria Swai | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 8. Mwl. Mtendeje Kingimali | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 9. Bw. Gerald Kauki | - | Mkuu wa Idara ya Maliasili |
| 10. Dkt. Feisal Said | - | Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe |
| 11. Bw. Oscar Myovela | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 12. Bw. Fabian P. Massawe | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 13. Bw. Sultan Kumbata | - | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 14. Bw. Bilsam Boniphas | - | Afisa Biashara |
| 15. Bw. Kabyemela Byabato | - | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi |
| 16. Bw. Richard Unambwe | - | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 17. Eng. Benny B. Komba | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 18. Mwl. Donesia Mwalukasa | - | Mkuu Mthibiti ubora wa Shule |
| 19. Bi. Julieth Mushi | - | Kny. Afisa Talafa |
| 20. Mwl. Elizabeth Kiraya | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |

Ufuatiliaji

SEKRETARIATI

1. Bw. Mongela O. Semhale

MUHTASARI NA. 11/2021/2022: KUFUNGUUA KIKAO

Akidi ilipotimia Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao ambapo Mwenyekiti alianza kwa kuwaambia Wajumbe kuwa kikao hiki ni kwa ajili ya kupitia taarifa za robo ya Kwanza 2021/2022. Baada ya ku sema hayo Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 05:20 Asubuhi.

MUHTASARI NA.12/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA

Menajementi ilipitia agenda za kikao na kuziridhia.

MUHTASARI NA. 14/2021/2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA COVID 19 TSH. 740,000,000.00 KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

Akiwasilisha taarifa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alisema Halmashauri ya Mji Handeni imepokea jumla ya fedha Tshs. 740,000,000.00 kutoka OR-TAMISEMI kwa kushirikiana Wizara ya Elimu Sayansi na teknolojia kupitia Mradi wa Mpango wa Maendeleo wa Mapambano dhidi ya COVID 19 kwa ajili ya Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa kwa Wanafunzi wa kidato cha kwanza na shule Shikizi kwa shule za Msingi na Sekondari. Fedha hizo zimeingizwa katika Akaunti za shule kama ifuatavyo:-

1. ELIMU MSINGI

NA	JINA LA SHULE SHIKIZI	IDADI YA MADARASA	KIASI
1	MNAZI MMOJA (SHULE MAMA NI MSASA)	3	60,000,000/=
2	KWEILALE (SHULE MAMA MAPINDUZI)	2	40,000,000/=
3	MANKINDA (SHULE MAMA NI KONJE)	2	40,000,000/=

4	K WAMNEKE	2	40,000,000/=
5	KOLOJA (SHULE MAMA NI KWEINUJUGO)	2	40,000,000/=
6	MABANDA (SHULE MAMA MISIMA)	2	40,000,000/=
7	BONDO (SHULE MAMA NI KWALUWALA	2	40,000,000/=
	JUMLA	15	300,000,000/=

2. SEKONDARI

NA	JINA LA SHULE	IDADI YA MADARASA.	KIASI
1	HANDENI SEKONDARI	2	40,000,000/=
2	KILELENI SEKONDARI	1	20,000,000/=
3	KIVESA SEKONDARI	2	40,000,000/=
4	KOMNYANG'ANYO	4	80,000,000/=
5	KONJE SEKONDARI	2	40,000,000/=
6	KWEDIYAMBA SEKONDARI	3	60,000,000/=
7	KWENUJUGO SEKONDARI	1	20,000,000/=
8	KATA YA MALEZI	2	40,000,000/=
9	MISIMA SEKONDARI	1	20,000,000/=
10	MSAJE SEKONDARI	4	80,000,000/=
	JUMLA	22	440,000,000.00

Pia Wajumbe walijulishwa kuwa, Halmashauri imepokea shilingi 90,000,000 za UVIKO – 19 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi (3 in 1) wa idara ya afya ambayo ujenzi wake unatakiwa uanze mara moja.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili kwa kina na kisha kuridhi, hata hivyo Mkurugenzi aliwaambia Wajumbe kuwa Ramani ya ujenzi wa Madarasa itabadilika badala ya Ofisi kukaa katikati ya madarasa itakuwa pembeni mwa madarasa na hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti.

MUHTASARI NA. 16/2021/2022: KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wa CMT nzima kwa michango mizuri na kisha alisisitiza wajumbe kujipanga katika kutekeleza miradi hii kwa njia ya Force Account na kuhakikisha inakamilika kabla ya tarehe 15/12/2021 kama maelekezo yalivyotolewa. Kisha alifunga kikao saa 09:06 Alasili.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA

KATIBU

MWENYEKITI

**JINA: BW. BONIFACE MADAY
SAINI.....**

**JINA: BI. MARYAM A. UKWAJU
SAINI:.....**

TAREHE:.....

